# COMPETENCY BASED CURRICULUM EXAM

PIONEER MARK SERIES

# GREDI YA SITA MWAKA- 2025

# KISWAHILI

**Jina:** ______________________________________________

**Shule:** ____________________ **Nambari ya usajili.** ________ **Tarehe:** _______

## VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHIMINI.

| KUZIDI MATARAJIO 41-50 | KUFIKIA MATARAJIO 25-40 | KUKARIBIA MATARAJIO 10-24 | MBALI NA MATARAJIO 1-9 | JUMLA (ALAMA %) 50 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1 – 5**

**MWALIMU** : Lisa acha! kabisa.
**LISA** : *(akikohoa)* Samahani mwalimu sikuona umefika.
**MWALIMU** : Mbona unafagia mahali penye vumbi hivi? Hujui vumbi ndiyo inakufanya ukohoe?
**LISA** : Mwalimu pana uchafu. Nimeona nifagie.
**MWALIMU** : Huongera kwa kuwajibika, Lisa. Lakini ni muhimu kuchunga afya yako pia.
**LISA** : Sawa mwalimu lakini ulitwambia tusikae katika mazingira machafu.
**MWALIMU** : Ni kweli Lisa nitakuonyesha jinsi ya kupunguza vumbi unapofagia.

**MASWALI**

1. Kwa nini Lisa alikuwa akifagia?
   A) Ili kuondoa vumbi
   B) Mwalimu alimtaka afagie
   C) Si vizuri kukaa kwenye mazingira machafu
   D) Ili mwalimu amuone
2. Mazungumzo haya kuna uwezekano yalifanyika wapi?
   A) Nyumbani C) hospitalini
   C) Shuleni D) kortini
3. Ni kwa nini Lisa alikuwa akikohoa?
   A) Alitaka ruhusa ya kwenda hospitalini
   B) Mwalimu alimwathibu
   C) Mazingira yake yalikuwa machafu
   D) Alikuwa akifagia mahali penye vumbi
4. Tunaweza kusema Lisa ni mwanafunzi ______________
   A) Mvivu B) mtiifu
   B) Mzembe D) mchangamfu
5. Taja msamiati wa adabu umetumika kwenye mazungumzo haya___________
   A) Hongera
   B) Acha!
   C) Mbona
   D) Samahani

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 6 hadi 10**

Turo na Turi ni marafiki sana. Wanapendana kama chanda na pete. Turo ni mrefu na mnene. Ana ngozi ya maji ya kunde. Turi ni mfupi kama nyundo. Yeye ni mweusi ti ti ti. Macho yake madogo yanapendeza. Turo na Turi wanaishi katika Kijiji Mato na wanasoma katika shule ya msingi ya Mwendo wa kasi. Turo ni Hodari katika somo la Hisabati. Turi naye ni hodari kwa mchezo wa kandanda. Wavulana hawa wawili wanatia bidii michezoni na masomoni. Mwalimu Moshi anawahimiza kuwa michezo ni muhimu kama vile masomo. Bi. Moshi hupenda kutoa mfano wa mwanariadha Kipchoge ambaye amefaulu maishani kwa ajili ya talanta yake ya mbio.

**Maswali.**

**6.** Turo na Turi walipendana kama chanda na pete. Je, ina maana gani?
- A) Wanapendaa kuvaa pete.
- B) Wanapendana sana
- C) Wanapendana kwa ajili ya pete
- D) Pete zao ni nzuri

**7.** Turo alikuwa hodari katika
- A) Hisabati
- B) Kandanda
- C) Riadha
- D) Kandanda na riadha

**8.** Mwalimu Moshi anawahimiza kuwa?
- A) Masomo ni bora zaidi kuliko michezo
- B) Ni vuzuri kutia bidii masomoni na kuacha michezo kabisa
- C) Michezo na masomo yote ni muhimu
- D) Michezo haiwezi kukufanya mtu wa maana

**9.** Turo na Turi ni __________
- A) Wavulana
- B) Mvulana na msichana
- C) Wasichana
- D) Walimu

**10.** Bi Moshi hupenda kutoa mfano wa nani? ____________
- A) Rais Ruto
- B) Kipchoge
- C) Turi
- D) Turo

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali (14 – 15)**

Kesho ni Ijumaa. Itakuwa sikukuu ya mashujaa nchini. Kutakuwa na sherehe ya kuadhimisha siku hiyo. Jena na Joana watakariri shairi kuhusu mashujaa. Tangu juzi wamekuwa wakifanya mazoezi ili kujiandaa. Mtondogoo watarejea shuleni watawasimulia wenzao kuhusu matukio ya siku hiyo.

**Maswali**

**11.** Jena na Joana watarejea shuleni mtondogoo. Mtondogoo itakuwa siku gani?
- A) Jumamosi
- B) Jumapili
- C) Jumatatu
- D) Jumanne

**12.** Mtu anayeipenda nchi yake huitwa?
- A) Kiongozi
- B) Mzalendo
- C) Katili
- D) Jasusi

**13.** Chagua vitendo vinavyoonyesha kuwa Jena na Joana wanapenda nchi yao.
- A) Kuhudhuria sherehe, kukariri shairi
- B) Kurejea shuleni kukariri shairi
- C) Kusimulia matukio, kuhudhuria sherehe
- D) Kusimulia matukio, kurejelea shuleni

**14.** Maana ya kujiandaa kulingana na kifungu hiki ni?
- A) Kujitambulisha
- B) Kujitayarisha
- C) Kujinufaisha
- D) Kujiburudisha

**15.** Mada ya shairi litakalokaririwa ni ipi?
- A) Kenya
- B) Mashujaa
- C) Jena na Joana
- D) Sikukuu

**Jaza pengo**

Musa ____16____ hospitalini tulienda ____17____ nyumbani ____18____. Alikuwa anaugua kichocho. Ugonjwa ____19____ kupitisha haja ____20____ damu.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 16. | Alipotoka | alitoka | alijitoa | akifika |
| 17. | Kumzika | Kumtembelea | kumwitia | kumjazia |
| 18. | Kwangu | kwetu | kwake | kwenu |
| 19. | Ya | za | la | wa |
| 20. | Yenye | zenye | penye | lenye |

**Kutoka swali la 21 – 30 jibu kulingana na maagizo**

**Jibu kitendawili hiki**

21. Kila mmoja anapitia mlango huo.
    A) Kifo B) Kanisa C) Darasa D) nyumba

**Andika sentensi ifuatayo katika wingi**

22. Chumba kile kidogo kimeangukia chungu.
    A) Chumba vile vidogo vimeangukia chungu
    B) Chumba vile kidogo vimeangukia chungu
    C) Vyumba vile vidogo vimeangukia vyungu

**Chagua aina ya nomino dhahania kwenye sentensi ifuatayo**

23. Gavana alieleza namna ya kupunguza umaskini
    A) Umaskini B) Gavana
    C) Namna D) alieleza

**Tumia kivumishi kiashiria kujaza nafasi**

24. Kitambaa ________kina madoadoa mengi mekundu.
    A) Kipya B) hiki C) kisafi D) change

**Andika katika hali ya ukubwa**

25. Mtoto mzuri anasoma
    A) Toto zuri linasoma
    B) Toto mzuri anasoma
    C) Kitoto kizuri kinasoma
    D) Kitoto zuri kinasoma

**Chagua nomino wingi katika sentensi hii**

26. Chai ilikuwa tamu ilipotiwa sukari
    A) Tamu B) ilipotiwa C) sukari D) ilikuwa
27. Tunapalilia mimea yetu. Aina gani ya kivumishi kilichopigiwa mstari?
    A) Kivumishi kiashiria B) Kivumishi cha sifa
    C) Kivumishi kimilikishi D) Kivumishi kihisishi
28. Ni kiungo kipi cha mwili huondoa uchafu kwenye damu?
    A) Mifupa B) Moyo C) Umio D) Figo
29. Kanusha: Mumara amesoma kitabu hicho
    A) Mumara hasomi kitabu hicho
    B) Mumara hatasoma kitabu hicho
    C) Mumara hakusoma kitabu hicho
    D) Mumara hajasoma kitabu hicho
30. Ni methali gani mwafaka kueleza kauli ifuatayo
    Jambo linaloshughulikiwa na wengi hufaulu
    A) Aliye juu mngoje chini
    B) Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi
    C) Pole pole ndio mwendo
    D) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

## INSHA

**Andika insha ya kusisimua**

**SIKU YA MICHEZO SHULENI**

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................